## MILANGO MINGI YA KUTATUA MGOGORO
***(MULTI-DOOR DISPUTE RESOLUTION)***

Kitengo hiki kinasaidia watu kutatua migogoro kupitia upatanishi na njia zingine za kututua mzozo.
Jengo la Mahakama A, Chumba 105
Simu: (202)879-1549

### Milango Mingi - CIRP
### Habari ya Jamii na Mpango wa Marejeo
***(Multi-Door – CIRP Community Information and Referral Program)***

CIRP ni mpango wa bure unaojaribu kuwasaidia watu watatue migogoro bila kupeleka kesi mahakamani.
Jengo la Mahakama A, Chumba 114

## MPANGO WA FIDIA WA WAATHIRI WA UHALIFU
***(CRIME VICTIMS COMPENSATION PROGRAM)***

Husaidia waathirika wa uhalifu wa mabavu na familia zao.
Jengo la Mahakama A, Chumba 109
Simu: (202) 879-4216

## VITUO VYA KUJISAIDIA NA MASHAURI*
***(Self-Help & Resource Centers*)***

Hizi vituo vinatoa habari ya kisheria ya bure kwa wale ambao hawana mawakili. Hawatoi msaada kwa njia ya simu kwa hivyo wale wanaotafuta msaada wanapaswa watembelee masaa ya kazi.

### Kituo cha Mashauri cha Madai Dogo
***(Small Claims Resource Center)***

Jengo la Mahakama B, Chumba 102
Masaa: Alhamisi, Saa tatu na robo mpaka saa sita adhuhuri (9:15a.m.-12: 00Noon)
Hutoa habari kuhusu sheria na utaratibu wa madai kwa wahusika.

### Kituo cha Mashauri ya Sheria za Ununuzi
***(Consumer Law Resource Center)***

Jengo la Mahakama B, Chumba 102
Masaa: Jumatano, saa tatu na robo mpaka saa sita adhuhuri (09:15-12: 00Noon)
Hutoa habari kuhusiana na masuala ya sheria ya watumiaji.

### Kituo cha Kujisaidia cha Mahakama ya Familia
***(Family Court Self-Help Center)***

Jengo la Mahakama la Moultrie, Chumba 4335 Simu: (202) 879-1471
Hutoa habari juu ya sheria ya familia kama vile talaka, ulezi, matembezi na kusimamia mtoto.

### Kituo cha Mashauri cha Wenye Nyumba na Wapangaji
***(Landlord Tenant Resource Center)***

Jengo la Mahakama B, Chumba 115
Simu: (202) 508 1710
Hutoa habari kwa makabaila na wapangaji walio na migogoro ya nyumba wasio na wakili.

### Kituo cha Mashauri ya Uthibitisho wa Wasia
***(Probate Resource Center)***

Jengo la MahakamaA, Ghorofa la 3
Simu: (202) 879-9460.
Hutoa habari na huduma za kisheria fupi kwa watu wasiye wakilishwa au watu wanaoweza kuhitaji huduma katika Kitengo cha Uthibitisho wa Wasia.

* Vituo vya Kujisaidia na Mashauri zinashughulikiwa na mashirika yasiyo ya faida, wanachama wa Sheria ya Mipango Isiolipiwa D.C. na wafanyakazi wa mahakama

### Ofisi ya Baraza la Wazee wa Mahakama Kuu D.C.
***(D.C. Superior Court Jurors' Office)***

500 Indiana Avenue, N.W., Room 3130
Washington, D.C. 20001
Simu: (202) 879-4604

### Huduma za Ufasiri *(Interpreting Services)*

Wafasiri wa bure waliohitimu kwa huduma za lugha zote za kuongea na za kuoneshwa. (202) 879-4828 (sauti)
Email: interpreters@dcsc.gov

### Msaada kwa Walemavu (ADA) *(Assistance for Persons with Disabilities )*

Huduma za bure zilizostahili, teknolojia, na vifaa kwa ajili ya watu wenye ulemavu wa kimwili au kiakili. (202) 879-1700 (sauti)
ADACoordinator@DCSC.gov

### Orodha ya TDD *(TDD Listing)*

| | |
|---|---|
| Jaji Mkuu wa Mahakama Kuu | (202) 879-1310 |
| Karani wa Mahakama ya Rufaa | (202) 626-8843 |
| Karani wa Mahakama Kuu | (202) 879-1232 |
| Kamati ya Kuingilia | (202) 626-8859 |
| Habari ya Kitengo cha Uhalifu | (202) 783-6445 |
| Ofisi Kuu | (202) 879-0105 |
| Habari ya Mahakama ya Jamii | (202) 879-0133 |
| Kitengo cha Wafanyakazi | (202) 879-4243 |
| Kituo cha Habari | (202) 879-1365 |

Braille Interpreter Large Print

**Mahakama ya Wilaya ya Columbia yanaingilika .**

### Ramani ya Majengo *(Building Location Map)*




**LENGO LETU**

Kulinda haki na uhuru, kutii na kuamua sheria, na kutatua migogoro kwa amani, haki na fanaka katika Mji Mkuu wa Nchi.

Rev. March 2011

**SWAHILI...**

# MAHAKAMA YA WILAYA YA COLUMBIA
## *(DISTRICT OF COLUMBIA COURTS)*

# HABARI *(INFORMATION)*



**Wazi kwa Wote * Kuaminiwa na Wote * Haki Zote**

**D. C. Mahakama ya Rufaa**
**Jengo la Mahakama la Kihistoria**
**430 E Street, NW**
**Washington, DC 20001**

**Mahakama Kuu ya Wilaya ya Columbia**
**Jengo la Mahakama la Moultrie**
**500 Indiana Ave., NW**
**Washington, DC 20001**

Jengo la Mahakama **A**
**515 5th Street, N.W.**
**Washington, D.C. 20001**

Jengo la Mahakama **B**
**510 4th Street, N.W.**
**Washington, D.C. 20001**

**(202) 879-1010**
**www.dccourts.gov**

Mahakama ya D.C, ni wazi Jumatatu-Ijumaa saa mbili unusu asubuhi mpaka sa kumi na moja jioni (8:30a.m.-5:00p.m.) isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo.

**MANENO MUHIMU**

**Pro Se:** Inamaanisha mtu anayewasilisha kesi bila mwanasheria.
**Mlalamishi:** Mtu ambaye anawasilisha malalamiko katika mashtaka.
**Mtuhumiwa:** Katika kesi ya kiraia, mtu anayeshtakiwa. Katika kesi ya jinai, mtu aliotuhumiwa na uhalifu.
**Mlalamikaji:** Mtu anayewasilisha malalamishi.
**Mushtakiwa:** Mtu anaye shtakiwa.
**Mkata rufaa:** Mtu anayekata rufaa katika Mahakama ya Rufaa.
**Mkatiwa rufaa:** Mtu ambaye rufaa inakatwa
**Hoja:** Ombi la matamshi au maandishi iliyotolewa na muhusika kabla, wakati, au baada ya kesi ambapo mahakama inatoa uamuzi au amri.

## MAHAKAMA KUU YA WILAYA YA COLUMBIA

***(SUPERIOR COURT OF THE DISTRICT OF COLUMBIA)***

Mahakama Kuu ndiye mahakama kwa kesi zote za eneo zinazohusu raia, ujinai, jamii, wasia na mambo ya kodi.

### MAMBO YA RAIA (*CIVIL MATTERS*)

**Tawi ya Mambo ya Raia (*Civil Actions Branch*)**

Tawi hii inashughulikia mambo ya raia katika Wilaya ya Columbia ambapo ile inayoleta mgogoro ni juu ya dola $ 5,000.
Jengo la Mahakama la Moultrie, Chumba 5000
Simu: (202) 879-1133
Masaa ya nyongeza ya kuwasilisha: Jumamosi saa tatu mpala saa sita adhuhuri (9:00a.m. -12Noon)

**Tawi la Mwenye nyumba na Mpangaji (*Landlord & Tenant Branch*)**

Tawi hii hushughulikia hatua za kumiliki nyumba na ukiukwaji wa kanuni ya makazi ya D.C. Jengo la Mahakama B, Chumba 110
Simu: (202) 879-4879; Kurekodi: (202) 879-1152 Masaa ya nyongeza: Jumamosi saa tatu asubuhi mpaka saa sita adhuhuri (9:00a.m.-12: 00Noon), Jumatano saa kumi na mbili unusu jioni mpaka saa mbili usiku (6:30p.m.- 8:00p.m.) (amri ya kulinda malipo tu)

**Tawi ya Madai Dogo na Upatanisho (*Small Claims & Conciliation Branch*)**

Tawi hi hushughulikia mchakato na hukumu wa makesi ambapo kiasi cha mgogoro ni $ 5000 au chini. Jengo la Mahakama B, Chumba 120
Simu: (202) 879-1120; Masaa ya nyongeza: Jumatano saa kumi na mbili unusu jioni mpaka mbili usiku (6:30 p.m- 8:00p.m), Jumamosi saa tatu asubuhi mpaka saa sita adhuhuri (9:00a.m.-12Noon)

### MAMBO YA UHALIFU (*CRIMINAL MATTERS*)

Majaji wa Kitengo cha Uhalifu husikiliza mambo yote ya uhalifu wa eneo ikijumuisha makosa madogo na makubwa, na kesi kubwa za barabarani.
Jengo la Mahakama la Moultrie: Chumba 4001
Simu: (202) 879-1373

**Tawi la Kesi Maalum** (*Special Proceedings Branch*)

Tawi hii inashughulikia hati za mahakama ya ujinai na mambo mengine maalum ya mahakama (watoro, washahidi wa kualikwa, uwezo wa akili, nk.)
Jengo la Mahakama la Moultrie Chumba 4002
Simu: (202) 879-1373

### MAMBO YA JAMII (*FAMILY MATTERS*)

Mahakama ya Familia ina mamlaka ya kisheria juu ya kesi zinazohusu madhulumu na utelekezaji , uhalifu wa vijana, mambo ya kinyumbani, uzazi na matunzo ya mtoto, afya ya akili, na ulemavu wa akili.

**Kituo Kuu cha Kuwasilisha (CIC) (*Central Intake Center*)**

CIC ni eneo moja ya kuwasilisha maombi mapya na yanayofuata kwa kesi za talaka, kutengana kisheria, ubatilishaji, ukaaji wa mtoto, upangaji mtoto, uhalili wa kufungwa, uzazi, utunzaji mtoto, uhalifu wa vijana, utelekezaji, hali ya akili na ulemavu wa akili.
Jengo la Mahakama la Moultrie, Chumba JM 520
Simu: (202) 879-1212

**Tawi ya Mambo ya Nyumbani (*Domestic Relations Branch*)**

Tawi la Mambo ya Nyumbani husimamia kesi za maombi ya talaka, ubatilishaji, kutengana kisheria, usimamizi, matembezi, mlezi wa ziada, hukumu za kigeni, maalishi ya mahakama za kigeni, upangaji mtoto, na kuondoa haki za wazazi.
Jengo la Mahakama la Moultrie, Chumba JM 300
Simu: (202) 879-1261

**Ofisi ya Ndoa (*Marriage Bureau*)**

Jengo la Mahakama la Moultrie, Chumba JM 4485
Simu: (202) 879-4840

**Tawi la Watoto na Utelekezaji (*Juvenile & Neglect Branch*)**

Jengo la Mahakama la Moultrie, Chumba JM 300
Simu: (202) 879-1465

**Tawi la Baba Mzazi na Utunzaji Mtoto (*Paternity & Child Support Branch*)**

Jengo la Mahakama la Moultrie, Chumba JM 300
Simu: (202) 879-4856

***Tawi la Hali ya akili na marekebisho (Mental Health & Mental Habilitation Branch)***

Jengo la Mahakama la Moultrie , Chumba JM 4475
Simu: 879-1040

### KITENGO CHA VURUGU NYUMBANI (*DOMESTIC VIOLENCE UNIT*)

Waamuzi katika Kitengo cha Uhasama Nyumbani husikiliza kesi ambapo wahusika wanaomba amri ya ulinzi wa kwanza dhidi ya watu wanaohusiana kwa damu, chini ya ulinzi wa kisheria, ndoa, wanao mtoto pamoja, wanaokaa pamoja (sasa au zamani), au kuwa na uhusiano wa kimapenzi (sasa au zamani).

Amri ya ulinzi wa muda ni halali kwa muda wa siku 14 na inaweza kupatikana katika moja kati ya hizi Vituo vya Kusikiliza Vurugu Nyumbani:

Jengo la Mahakama la Moultrie, Chumba 4400
Simu: (202) 879-0157

United Medical Center
1328 Southern Ave., SE, Room 311 Washington, DC 20032
Simu: (202) 561-3000

### MAMBO YA UTHIBITISHO WA WASIA (*PROBATE MATTERS*)

Kitengo cha Uthibitisho wa Wasia ina mamlaka juu ya wasia, mali ya watu waliofariki, hazina, usimamizi wa watoto, na uchungaji wa watu wasiojiweza.
Jengo la Mahakama A, Ghorofa la 3
Simu: (202) 879-4800

## MAMBO YA KODI (*TAX MATTERS*)

Kitengo cha Kodi kinashughulikia rufaa zote na mawasilisho ya kurejewa ya Wilaya ya Columbia kuhusu utathmini wa kodi na mielekeo yote ambapo Wilaya inapendekeza adhabu ya kijinai chini ya kanuni za kodi za D.C.
Jengo la Mahakama la Moultrie,
Chumba 3131 Simu: (202) 879-1737

### HAKIMU CHUMBANI (*JUDGE-IN-CHAMBERS*)

Hakimu Chumbani anawajibu kwa mambo mbalimbali ya dharura wakati wa masaa ya biashara ya kawaida inayohitaji uamuzi wa haraka. Haya mambo ya dharura hutoka kutoka vitengo vyote vya Mahakama na inajumuisha agizo za Amri ya Uzuizi wa Muda. Jengo la Mahakama la Moultrie, Chumba 4220
Simu: (202) 879-1450

## MAHAKAMA YA RUFAA YA WILAYA YA COLUMBIA

***(DISTRICT OF COLUMBIA COURT OF APPEALS)***

Mahakama ya Rufaa D.C. ni sawa na mahakama ya juu ya jimbo. Kama mahakama ya juu kabisa ya Wilaya ya Columbia, mahakama ina mamlaka ya kupitia maagizo yote ya mwisho, hukumu na baadhi ya amri zisiyo za mwisho za Mahakama kuu. Mahakama pia ina mamlaka ya kupitia maamuzi ya wakala wa utawala, halmashauri, na tume za Wilaya ya utawala Columbia, pamoja na kujibu maswala ya kisheria iliyothibitishwa na mahakama ya rufaa ya nchi na jimbo.

Ukipoteza kesi yako katika Mahakama Kuu unaweza kukata rufaa kwa Mahakama ya Rufaa D.C.

Agizo ya Hakimu lazima ipitiwe na Jaji wa Mahakama Kuu kabla ya kukatiwa rufaa katika Mahakama ya Rufaa ya Wilaya ya Columbia.

Mawasiliano: Ofisi ya Umma
Simu: (202) 879-2701


Wazi kwa Wote * Kuaminiwa na Wote * Haki Zote kwa Wote
Wazi kwa Wote * Kuaminiwa na Wote * Haki Zote kwa Wote

Swahili, Rev. February 2011